

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**



TAARIFA KWA UMMA

**DKT. PHILIP MPANGO: KITUO CHA UTAFITI NALIENDELE MKOANI
MTWARA KUPEWA FEDHA ZA KUTOSHA**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dkt. Philip Mpango, ameuahidi uongozi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo Naliendele kwamba Serikali itakiwezesha Kituo hicho na vituo vingine vya utafiti nchini ili viendeleze kazi ya utafiti wa mazao ya kilimo ambacho kinategemewa na watanzania wengi katika kujikwamua kiuchumi.

Dkt. Mpango ametoa ahadi hiyo alipotembelea Kituo cha Utafiti Naliendele, mkoani Mtwara, ambacho uongozi wake ulielezea wasiwasi wake wa kupata rasilimali fedha za kuendeleza utafiti wa mazao likiwemo zao la korosho pamoja na watumishi baada ya kuondolewa kwa fedha za ushuru wa korosho inayouzwa nje, zilizokuwa zikitumika kuendeleza utafiti huo.

Alisema kuwa Serikali inatambua umuhimu wa shughuli za utafiti katika kuendeleza uchumi na maendeleo ya nchi kwa ujumla na kwamba atajitahidi kama Waziri wa Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Waziri mwenzake anayeshughulikia kilimo ili taasisi hiyo isikwame kufanya shughuli zake.

"Niwahakikishie kabisa kwamba Serikali haitakubali utafiti wa mazao yote unaofanyika hapa likiwemo zao la korosho udhurike, litakuwa ni janga kubwa, kwahiyo upatikanaji wa fedha za Kituo hiki litakuwa ni moja ya vipaumbele vyangu" alisisitiza Dkt. Mpango

Alisema kuwa kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa na kwamba hakutakuwa na mapinduzi ya viwanda bila kilimo kwa sababu viwanda vinavyojengwa vinarajiwa kuongeza thamani ya mazo ya kilimo pamoja na mazao ya mifugo na uvuvi.

Awali, Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo Naliendele, Dkt. Omari Mponda, alieleza kuwa Kituo chake kinahitaji zaidi ya shilingi bilioni 7 kwa mwaka ili kiweze kuendeleza shughuli za utafiti hasa baadaya Serikali kuamua kupanua shughuli za utafiti wa zao la korosho kwenye mikoa mingine nchini.

Alisema kuwa hivi sasa Kituo kimeelekeza nguvu zake katika utafiti wa ugonjwa mpya unaoathiri kwa kiwango kikubwa zao la korosho ujulikanao kama mnyauko

fusari (Fusarium wilt) , ulioathiri zao hilo katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Mkuranga, Masasi, Tandahimba, Mtwara na Liwale, lakini changamoto kubwa inayowakumba ni ukosefu wa fedha za kuendeleza utafiti huo.

"Mheshimiwa Waziri, Kituo hiki pia kina zaidi ya asilimia 50 ya watumishi ambao wameajiriwa kwa njia ya mikataba na wanahitaji kulipwa vizuri ili wabaki Kituoni hapa kuendeleza shughuli za utafiti ndio maana nasema tuna mahitaji makubwa ya fedha na tunaomba Serikali iliangalie jambo hili" Alisema Dkt. Mponda.

Kituo cha Utafiti Naliendele kilichoko mkoani Mtwara kinatajwa kuwa ni kitovu cha utaalamu wa zao la korosho katika Bara la Afrika na kwamba tafiti nyingi, ikiwemo aina 54 za mbegu za zao la korosho kunakifanya kituo hicho kuwa tegemeo kwa masuala ya utafiti katika nchi nyingi za afrika ambazo hutumia Taasisi hiyo kupata teknolojia ya uzalishaji wa mbegu bora za mazao mbalimbali hususan korosho.

Imetolewa na;

Benny Mwaipaja
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Fedha na Mipango